# JARIDA LA USHIRIKA

OKTOBA 2023- MACHI 2024

## MAFANIKIO SEKTA YA USHIRIKA KATIKA MIAKA MITATU YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA








# YALIYOMO


- KUTOKA KWA MRAJIS ............ 03
- MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA............ 04- 08
- RUNALI WAJENGA KIWANDA CHA KUKAMUA MAFUTA ............ 08
- UWAZI MIKATABA YA USHIRIKA KUONGEZA TIJA ............ 09
- SACCOS MKOMBOZI WA UCHUMI KWA WANAWAKE ............ 10
- MAADHIMISHO YA WIKI YA VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO ............ 11
- KONGAMANO LA SACCOS BARANI AFRIKA............ 12
- MRAJIS ATOA ONYO KWA VIONGOZI WA VYAMA WASIOFUATA SHERIA ... ............ 13
- DC MTWARA AVITAKA VYAMA VYA MSINGI KUHARAKISHA MALIPO KWA WAKULIMA ............ 14
- SACCOS ZATAKIWA KUJIUNGA NA SCCULT ... ............ 16
- HAKIKISHENI VIPAUMBELE VYA TUME VINATEKELEZWA ............ 18
- VIONGOZI WA VYAMA WATAKIWA KUTOKUTANGULIZA MASLAHI BINAFSI ............ 19
- AMCOS TABORA ZAMPONGEZA RAIS SAMIA ............ 20
- RAMADHAN MIRAJI MWENYEKITI TCDC SACCOS ............ 22
- JENGO JIPYA LA CHAMA KIKUU LINDI MWAMBAO LAZINDULIWA ............ 23
- SHAMBA LA MAMCU LAZINDULIWA ............ 24
- NAIBU WAZIRI AZINDUA MATUMIZI YA MIZANI ZA KIDIGITALI KATIKA UNUNUZI WA MAZAO. .25
- MAMCU YACHANGIA MIL. 75 UJENZI WA MADARASA ............ 26
- CHAMA KIKUU KARAGWE CHAZINDUA MIRADI YA MAENDELEO ............ 28
- KACU YAPONGEZWA KWA KULIPA MKOPO WA KUNUNUA PAMBA ............ 29
- MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA .... ............ 30
- ANUANI ZA OFISI ZA TCDC MIKOANI............ ............ 31 - 32


**UKURASA WA MBELE**





Dkt. Benson Ndiege, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)

# Kutoka kwa Mrajis

Ni wakati mwingine ambapo Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) inakuletea Jarida la Ushirika Toleo la 15 ambalo ni sehemu ya kukuhabarisha na kukupa fursa ya kuelewa jitihada nyingi zinazofanyika katika kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Ushirika.

Tume imeendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa Sekta ya Ushirika inakuwa na kuimarika ambapo ukuaji wa Sekta hadi kufikia mwezi Juni 2023, imesajili jumla ya Vyama vya Ushirika **7,300;** kati ya hivyo, **77** ni Vyama vya Upili, 1 ni Shirikisho la Vyama vya Ushirika, **4,252** ni Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), 2,034 ni Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) na **936** ni Vyama vinavyojishughulisha na kazi mbalimbali zikiwemo, ufugaji na uvuvi.

Aidha, idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka wanachama **6,965,272** Disemba, 2021 hadi **8,358,326** kufikia Machi, 2023. Ongezeko hilo limetokana na uhamasishaji wa umuhimu wa wananchi kujiunga na ushirika ili kuwawezesha kupata nguvu ya pamoja ya soko na mitaji.

Katika ukuaji wa Sekta ya Ushirika natoe rai kwa Vyama vya Ushirika ambavyo vinaendelea na taratibu za uchaguzi wa Viongozi kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za Ushirika ili Sekta hii iendelee kukua kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora na Weledi. Chaguzi hizi za Viongozi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 imeelekeza Bodi za Vyama vya Ushirika hupaswa kukaa madarakani kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu (3) lakini Wajumbe/Mjumbe wanaweza kuchaguliwa tena kuhudumia kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu (3).

Tume imetoa Waraka wa Mrajis Na.2 wa Mwaka 2023 ambao pamoja na mambo mengine umeelekeza Wajumbe wa Bodi ya Uongozi wa Chama cha Ushirika watatakiwa wawe kati ya watano (5) hadi tisa (9) kwa kuzingatia shughuli za Chama husika na uwezo wake wa kiuchumi. Nitumie fursa hii kuwakumbusha kuwa ni vema idadi ya Wajumbe watakaochaguliwa iwe ile isiyogawanyika kwa mbili (2) yaani; 5,7 au 9 ili kuondoa mivutano pale Bodi ya Chama husika itakapotaka kufanya maamuzi.

Aidha, Tume katika kuhamasisha Wanawake kushiriki nafasi za Uongozi imeelekeza katika Waraka wa Mrajis wa Uchaguzi kuwa katika idadi ya Wajumbe wa Bodi na Kamati ya Usimamizi watakaochaguliwa, wanawake watakuwa na idadi isiyopungua theluthi moja (1/3) ya Wajumbe wa Bodi yote ya Chama husika.

Nitoe wito kwa Vyama vyote vya Ushirika vyote vinavyoendelea na taratibu za Chaguzi za Viongozi wa kuzingatia Sheria na Maelekezo yote muhimu yanayotolewa ili kupata viongozi Bora, waadilifu na wachapa Kazi kwa maendeleo ya Sekta ya Ushirika.

*Nawatakia Kila la Heri!*

# MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA KATIKA MIAKA MITATU (2021/2022 - 2023/2024) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika ni Idara ya Serikali inayojitegemea iliyo chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ili kutekeleza majukumu ya Udhibiti na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika pamoja na Uhamasishaji wa Maendeleo ya sekta ya Ushirika nchini.

**Majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Majukumu makuu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika ni pamoja na: Kuandikisha na kufuta vyama vya ushirika; Kukagua na Kusimamia vyama vya ushirika; Kutunza na kuboresha rejista ya vyama vya ushirika; Kutatua migogoro na malalamiko katika vyama vya ushirika; Kuhimiza na kuhamasisha maendeleo endelevu na ya kiuchumi ya vyama vya ushirika; Kutoa elimu na mafunzo kwa wanachama na watumishi wa vyama vya ushirika kuhusu uendeshaji wa ushirika; Kukusanya, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa za vyama vya ushirika; na Kufanya tafiti mbalimbali kwa maendeleo ya vyama vya ushirika.

**MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA**

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Awamu ya Sita ya Serikali (2021/2022 - 2023/2024) inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Ushirika imepata mafanikio katika maeneo yafuatayo:

**1. Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika**

Tume imefanya kaguzi kwenye Vyama vya Ushirika ambapo imebainika kuwepo kwa kuimarika katika utendaji wa vyama vya ushirika kama inavyoonekana katika matokeo ya Kaguzi za mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023.

**Hali ya Kaguzi katika Vyama vya Ushirika**

| S/N | HALI YA UKAGUZI | 2021/2022 | 2022/2023 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Hati safi | 339 | 479 | 41.30 (zimeongezeka) |
| 2. | Hati zenye shaka | 2,393 | 2,475 | 3.43 (zimeongezeka) |
| 3. | Hati isiyoridhisha na maoni | 1,198 | 127 | 89.40 (zimepungua) |
| 4. | Hati mbaya | 2,075 | 830 | 60 (zimepungua) |

Kuimarika kwa vyama kumechangiwa na jitihada za Tume kwa kuongeza vitendea kazi, ambapo hadi kufikia mwaka 2023/ 2024 Tume imenunua magari 15 katika Ofisi za Mikoa ukilinganisha na magari 7 yaliyokuwepo mikoani mwaka 2021/2022. Aidha, mafunzo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika yametolewa kwa Maafisa Ushirika katika mikoa 20, Watendaji wa Vyama vya Ushirika 7,517, Wanachama 40,253 na Viongozi 5,553.




***Baadhi ya magari yaliyonunuliwa na TCDC na kupelekwa katika Ofisi za Tume za mikoa kwa ajili ya Usimamizi na Uhamasishji wa Maendeleo ya Ushirika***

**2. Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Vyama vya Ushirika**

Katika kuimarisha uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, Tume ilifanya zoezi la ukaguzi wa sifa za watendaji wakuu wa Vyama Vikuu vyote vya Mazao na Miradi ya Pamoja 50 na kubaini kuwa asilimia 35 tu ya watendaji wakuu walikuwa na sifa stahiki. Kupitia maelekezo ya Tume, Vyama Vikuu vinne (4) vya IGEMBENSABO, PMCU, ACU, na KICU vimeajiri watendaji wapya, na Vyama 11 vya KYECU, TAMCU, SORECU, CHUTCU, SORECU, TAMCU, MAMCU, TANECU, RIVACU, SIFACU na LATCU vimeomba vibali vya ajira kwa watendaji wake.

**3. Usimamizi wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha (SACCOS)**

Tume katika kusimamia Vyama vya Ushirika vya kifedha (SACCOS), mafanikio yafuatayo yamepatikana; ambapo hadi kufikia Desemba 2023, mali za SACCOS ziliongezeka na kufikia Shilingi Trilioni 1.3 kutoka Shilingi Trilioni 1.22 mwaka 2022. Jumla ya Akiba na Amana zimeongezeka na kufikia Shilingi Billioni 980 kutoka Shilingi Billioni 897 mwaka 2022. Jumla ya Mikopo inayodaiwa imeongezeka na kufika Shilingi Trilioni 1.1 kutoka Shilingi Trilioni 1.05 mwaka 2022. Mtaji tete umeongezeka na kufikia Shilingi Billioni 214.7 na kutoka Shilingi Bilioni 203 mwaka 2022.

**Mafanikio ya SACCOS**

| Maelezo | Mwaka 2022 | Mwaka 2023 |
|---|---|---|
| | Shilingi | Shilingi |
| Mali za SACCOS | Trilioni 1.22 | Trilioni 1.3 |
| Akiba na Amana | Bilioni 897 | Bilioni 980 |
| Mikopo inayodaiwa | Trilioni 1.05 | Trilioni 1.1 |
| Mtaji tete | Bilioni 203 | Bilioni 214.7 |

**4. Vyama vya Ushirika kutumia mifumo rasmi ya masoko ya mazao ya wakulima**

Wakulima wameendelea kukusanya na kuuza mazao yao kupitia mfumo rasmi wa masoko kupitia Vyama vya Ushirika. Katika mwaka 2023/2024 hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Tani 779,958 zenye thamani ya Shilingi 1,835,977,350,938 zilikusanywa na kuuzwa kupitia mfumo rasmi wa Ushirika ukilinganisha na Tani 597,298.58 zilizouzwa kwa thamani ya Shilingi 1,552,635,769,446 mwaka 2021/2022. Thamani ya mauzo imeongezeka kwa asilimia 18.25. Mazao yaliyouzwa kupitia Ushirika ni tumbaku, korosho, pamba, kahawa, ufuta, kakao, mkonge, chai, mbaazi, soya, zabibu, miwa na maharage.

Thamani ya mazao yaliyouzwa kupitia Ushirika

| Na. | | 2021/2022 | 2023/2024 |
|---|---|---|---|
| 1. | Uzito kwa Tani | 597,298.58 | 779,958 |
| 2. | Thamani (Shilingi) | 1,552,635,769,446 | 1,835,977,350,938 |

Aidha, kupitia Mfumo wa Mauzo ya Moja kwa Moja (Direct Sales), Vyama Vikuu vya Ushirika vya KCU (1990) Ltd na KDCU Ltd vya Mkoani Kagera, vimeendelea kuuza Kahawa Hai (organic coffee) katika Soko la Haki (Fair Trade Market). Hadi kufikia Februari 2024, jumla ya Kilo 4,813,850 za Kahawa Hai ambayo ilikuwa haijasagwa (coffee beans) na kahawa hai iliyosagwa (instant coffee), ziliuzwa kupitia Soko la Haki katika nchi za Ujerumani, Japani, Ubeligiji, Canada, China na Amerika ya Kaskazini kwa thamani ya Shilingi 30,576,880,548.90, ikilinganishwa na mauzo ya Kilo 1,797,722 zenye thamani ya Shilingi 10,801,014,641.00 zilizouzwa mwaka 2022/2023.



***Moja ya Minada ya mazao yanayouzwa kupitia Mfumo wa Ushirika na Stakabadhi za Ghala mkoani Mtwara***

**Mauzo ya Kahawa hai iliyouzwa na vyama vya KDCU NA KCU**

| BIASHARA YA KAHAWA HAI KATIKA SOKO LA HAKI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| AINA YA KAHAWA | 2022/2023 | | 2023/2024 | |
| KG | THAMANI(TSH) | KG | THAMANI(TSH) | |
| ISIYOSAGWA | 1,612,540 | 10,391,207,760.00 | 4,640,400 | 30,162,013,29 8.90 |
| ILIYOSAGWA | 185181.6 | 409,806,880.80 | 173,450 | 414,867,250.00 |
| **JUMLA KUU** | **1,797,722** | **10,801,014,641.00** | **4,813,850** | **30,576,880,548.90** |

### 5. Upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kupitia Vyama vya Ushirika

Katika msimu wa 2023/2024, jumla ya pembejeo zenye thamani ya Shilingi 307,673,032,600.00 zilinunuliwa kupitia Vyama vya Ushirika na kusambazwa kwa wakulima ikilinganishwa na pembejeo zenye thamani ya Shilingi 9,010,403,964.00 kwa mwaka 2021/2022. Aina za pembejeo zilizonunuliwa na kusambazwa kwa wakulima ni mbolea, viuatilifu (madawa), vifungashio, mbegu na miche kwa ajili ya mazao ya kahawa, pamba, korosho, mahindi, ufuta, alizeti, tumbaku na mpunga.

Aidha, katika mwaka 2023/2024, Vyama 776 vilipata vibali vya kununua na kusambaza mbolea kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), ikilinganishwa na Vyama 22 katika mwaka 2021/2022. Jumla ya Mifuko 117,926 ya Mbolea ya Ruzuku yenye Ujazo wa Kilo 50 ikiwa na Uzito wa Tani 6,444 na thamani ya Shilingi 8,346,750,968, imenunuliwa na Vyama vya Ushirika kati ya Tani 60,882 zilizonunuliwa na kusambazwa katika katika sekta ya kilimo kupitia Mfumo wa ruzuku.

**Usambazaji wa Pembejeo**

| USAMBAZAJI WA PEMBEJEO KUPITIA VYAMA VYA USHIRIKA | | |
|---|---|---|
| PEMBEJEO | Thamani ya Mauzo (Shilingi) | |
| | 2021/2022 | 2023/2024 |
| MBOLEA | 6,018,386,364.00 | 12,178,621,500.00 |
| MBEGU na VIUATILIFU | 860,645,250.00 | 285,882,871,035.00 |
| VIFUNGASHIO | 2,050,135,850.00 | 9,328,015,550.00 |
| MICHE | 81,236,500.00 | 283,524,515.00 |
| **JUMLA** | **9,010,403,964.00** | **307,673,032,600.00** |

### 6. Viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika

Vyama vya Ushirika vinamiliki jumla ya viwanda 328; kati ya viwanda hivyo, viwanda vinne (4) vya kuchambua na kuchakata Pamba vya KACU Ltd (Shinyanga), MBCU Ltd (Geita), CCU Ltd (Chato) na SOLA (SIMCU Ltd Simiyu) vimefufuliwa ili kuongeza thamani na bei ya zao hilo katika soko. Aidha, viwanda viwili (2) vya kuchakata kahawa vimefanyiwa matengenezo, KDCU LTD (Kagera) na WAMACU LTD (Mara); na viwanda vipya vitatu (3) ambavyo ni vya kiwanda cha kukamua mafuta ya Mbegu cha Chama cha RUNALI, Kiwanda cha vifungashio cha SONAMCU na Kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU LTD vimekamilika mwaka huu 2024.



*Kiwanda cha kubangua Korosho kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika TANECU*

### 7. Ajira katika Vyama Vya Ushirika

Kuimarika kwa Vyama vya Ushirika kumefanikisha kuongezeka kwa wananchi walioajiriwa katika vyama hivyo kufikia 153,982 mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na wananchi 100,100 waliopata ajira katika vyama mwaka 2020/21, ikiwa ni ongezeko la asilimia 53.8.

### 8. Kukuza matumizi ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika

**» Matumizi ya MUVU**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetengeneza Mfumo wa kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambao ulizinduliwa mwezi Julai 2023. Lengo la MUVU ni kuimarisha usimamizi, kuboresha ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango mbalimbali ya maendeleo katika kukuza sekta ya Ushirika kwa ujumla.

Hadi Machi 2024, vyama vya ushirika 6,134 vimesajiliwa kwenye MUVU kati ya vyama 7,468 vilivyo kwenye Daftari la Usajili wa Vyama, na jumla ya Vyama 1,843 vimeanza kutumia MUVU katika shughuli za uendeshaji. Aidha, jumla ya Mali 9,106 za Vyama Vikuu vya Ushirika zenye thamani ya Shilingi 2,023,167,983,761 zimefanyiwa utambuzi na kuingizwa kwenye MUVU.

Mfumo huu umeunganishwa na Mifumo mingine mitano (5) ambayo ni Mfumo Mkuu Unganishi wa Serikali (GovESB), Mfumo wa Mizani ya Kielekroniki ya Upimaji wa Mazao (Mkulima Hub), Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Rasilimali (ERMS), Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG) na Mfumo wa Usajili wa Watu kwa njia ya Mtandao



chini Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

***Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akizindua Mfumo wa kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU)***

**» Mizani za Kidigitali**

Tume imesimamia mchakato wa upatikanaji wa Mizani ya Kidijitali kwenye vyama vya ushirika ambapo jumla ya Mizani za Kidijitali 1,178 zenye thamani ya Shilingi 3,534,000,000.00 zilinunuliwa na kusambazwa kwenye Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) vinavyojishughulisha na mazao ya kahawa, korosho, ufuta, soya, mbaazi, kakao na tumbaku katika Mikoa ya Kagera, Lindi, Mbeya, Tabora,



Mtwara, Ruvuma na Pwani.

### 9. Kuhamasisha Uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika

Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kuhamasisha wadau mbalimbali kununua Hisa ili kupata Mtaji wa Shilingi Bilioni 20 unaohitajika kuanzisha rasmi Benki hiyo. Kupitia uhamasishaji uliofanyika, uwekezaji katika Hisa umeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 4.7 Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kufikia Shilingi Bilioni 15.7 mwezi Februari, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 236. Vyama vya Ushirika vimewekeza jumla ya Shilingi Bilioni 7.3 sawa na asilimia 72 ya kiasi cha Shilingi Bilioni 10.2 kilichotengwa kwa ajili ya Vyama vya Ushirika kuwekeza na kumiliki Hisa kwa asilimia 51.




Benki hiyo inatarajiwa kuzinduliwa rasmi ifikapo Mei, 2024.

***Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL)***

### 10. Kuvipanga Vyama vya Ushirika visivyo vya Kifedha kwenye Madaraja

Katika kuviwezesha Vyama kujiendesha kibiashara, Tume imeanza mchakato wa kupanga vyama kwenye madaraja. Hadi sasa, Tume imeandaa kigezo cha

kupanga Vyama katika madaraja. Kigezo hicho kimeweka madaraja matatu (Daraja A, Daraja B na Daraja C) kwa kutumia kigezo cha ukubwa wa mali. Lengo ni kuweza kutambua ukubwa wa chama na kuweka utaratibu bora wa kuvisimamia. Aidha, imetengeneza kigezo cha ufanisi kitakachogawa vyama kwenye madaraja 4 (Utendaji Bora; utendaji mzuri sana; utendaji wa kuridhisha na utendaji dhaifu). Upangaji vyama kwenye Madaraja utafanyika kwenye MUVU baada ya kuingizwa taarifa za utendaji wa vyama.

**11. Kujenga Taswira Chanya ya Ushirika (Branding of Cooperatives Model)**

- Tume imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano (Communication Strategy) na Mwongozo wa Mawasiliano kwa Tume na vyama kwa kufanya yafuatayo:
- Tume inatumia kikamilifu Mitandao ya kijamii (facebook, Instagram), tovuti na Vyombo vya Habari kuhabarisha umma kuhusu yanayotokea kwenye ushirika kila siku; Vyama vimeanza kutangaza mafanikio yake kupitia mikutano mikuu ya vyama kwa kushirikiana na Vyombo vya Habari. Aidha, baadhi ya vyama (kama vile TANECU, KACU, KDCU, WAMACU, RUNALI, SONAMCU, MAMCU, TAMCU, LINDI MWAMBAO,) na baadhi ya SACCOS ikiwemo BANDARI, TANESCO, NGOME, URA na KKKT - ND) na Benki ya Ushirika Kilimanjaro vimeanza kutumia Vyombo vya Habari na social media kutangaza shughuli zake; na

Tume kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika inatangaza mafanikio ya Ushirika kwenye Majukwaa ya Ushirika ya kila mkoa na kilele chake hufanyika kitaifa kwenye Siku ya Ushirika Duniani (SUD) na Maadhimisho ya Siku ya Ushirika wa Kifedha Duniani (ICUD).



***Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege akizungumza na Waandishi wa Habari Jijini Dodoma***

## WAZIRI BASHE AFANYA KIKAO NA VIONGOZI WA WIZARA YA KILIMO NA TAASISI ZAKE

Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe, Oktoba 31, 2023 amefanya Kikao Kazi na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi za Wizara, Menejimenti ya Wizara pamoja na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Wizara ya Kilimo.

Waziri Bashe amekutana na Viongozi hao Jijini Dodoma katika kikao kazi cha pamoja cha kupitia Dira ya pamoja ya Wizara ya Kilimo ili kuwezesha malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Kilimo kufikiwa.



***Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (Mb) akiongea na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi, Menejimenti na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Wizara ya Kilimo katika kikao kazi kilichofanyika Oktoba 31, 2023 Jijini Dodoma.***

## RUNALI WAJENGA KIWANDA CHA KUKAMUA MAFUTA CHENYE THAMANI YA SHILINGI 143,816,000

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, amekipongeza Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale RUNALI LTD kwa kujenga Kiwanda cha kukamua mafuta chenye Thamani ya Shilingi 143,816,000 ambacho kitaongeza thamani ya mazao ya wanachama wao pamoja na wakulima kwa ujumla kwa kutumia mapato ya ndani.

Amesema hayo tarehe 07 Desemba, 2023 wakati akifungua Kiwanda hicho ambapo ameeleza kupitia mradi huu wa kiwanda hicho Chama kitaenda kuongeza thamani ya mazao ya wakulima ambayo hapo awali yalikuwa yanauzwa yakiwa ghafi.

"Sasa niwaombe watendaji na wasimamizi watakaoajiriwa katika kiwanda hiki kufanya kazi kwa ufanisi na weledi ili kiwanda hiki kiweze kuwa na tija

kwa wakulima wetu maana hii ni fedha ya wakulima wetu," amesema Dkt. Ndiege.



***Mrajis wa Vyama vya Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt.Benson Ndiege (katikati) akizindua Kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti kilichojengwa na Chama kikuu cha RUNALI LTD Disemba 07,2023***

Pia amewapongeza RUNALI namna ambavyo wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa kusimamia malipo ya wakulima kwa wakati hasa katika vipindi vya mauzo ya mazao kwa kipindi cha miaka ya karibuni na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeshuhudia kupungua kwa migogoro hasa kipindi cha misimu ya mauzo ya mazao.



***Kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti kilichojengwa na Chama Kikuu cha Ushirika RUNALI LTD na kilichozinduliwa Desemba 07, 2023***

"Hii inaonesha kuwa usimamizi pamoja na weledi kwenye Vyama vya Ushirika unaendelea kuimarika zaidi," amesema Mrajis.

Naye Afisa Masoko wa RUNALI, Beatrice Liungulu, amesema mradi huu unatarajia kunufaisha wakulima zaidi ya 30,000 wanaohudumiwa na Chama cha RUNALI kwa kuongeza kipato kupitia zao la Alizeti hivyo kuendelea kuhamasisha kilimo cha Alizeti kwasababu linaweza kulimwa na mazao mengine kwenye shamba moja.

Pia Beatrice amesema kupitia Mradi huo Kiwanda kitazalisha mafuta halısı ya kupikia yanayotokana na mbegu mbalimbali ikiwemo Alizeti, Ufuta, Karanga na Mbegu za Maboga ambayo yatapatikana kwenye ujazo wa lita tano, lita tatu lita moja na nusu lita.

## UWAZI MIKATABA YA USHIRIKA KUONGEZA TIJA



***Moja ya mikataba ya Ushirika ikasiniwa Mkoani Kilimanjaro.***

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege, amevitaka Vyama vya Ushirika kufanya Mikataba kwa uwazi kwa kuhusisha wadau husika na Mikataba hiyo ili kuepusha uwezekano wa Migogoro.

Dkt. Ndiege ametoa kauli hiyo wakati wa Mkutano na Wanaushirika wa utiaji Saini wa Mkataba kati ya Ushirika wa Mradi wa Pamoja wa Murosang na Muwekezaji wa Mashamba Kampuni ya McJaro Ltd akiwa katika Ziara ya kikazi Wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro Machi 12, 2024

Mrajis amesema Vyama vihusishe wadau na Wataalamu mbalimbali kwa kupata Ushauri na kuelewa Mikataba kabla ya kusaini ili kuepusha migogoro inayotokana na kutoelewa masharti ya baadhi ya Mikataba na kuongeza kuwa Mikataba hiyo isainiwe kwa kuwaalika Wanachama na Wadau wa Chama kwa Uwazi na ikiwezekana iwe kwa lugha ya Kiswahili.

"Nitoe wito kwa Vyama msijifungie wenyewe peke yenu Mkaingia Mikataba bila kuwa na uelewa sahihi, iteeni Wataalamu pale mnapohitaji msaada na hata siku ya kusaini iteni Wanachama na Wadau washuhudie kama tunavyofanya leo hii," alisema

"Kama Mkataba upo kwa lugha ya Kiingereza basi hakikisheni kuwa Mkataba huo pia ikiwezekana uwe na lugha ya Kiswahili ili watu wauelewe na kama kuna

jambo la ufafanuzi ulizeni na Ofisi yangu itawapa ushirikiano pale mnapouhitaji," amesisitiza

Sambamba na hilo nae Mbunge wa Jimbo la Hai Mhe. Saashisha Mafuwe katika Mkutano huo ametoa rai kwa Wanaushirika kuhamasisha Vijana kuingia katika Vyama vya Ushirika ili kuwa na uendelevu wa Vyama na kuongeza kasi, tija na ustawi wa Vyama vyenye ubunifu na muelekeo chanya Kiuchumi.

## SACCOS MKOMBOZI WA UCHUMI KWA WANAWAKE - DC NYAMAGANA




***Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Mheshimiwa Amina Makilagi akizungumza wakati wa Kongamano la Jukwaa la Wanawake wa SACCOS Kitaifa lililofanyika Jijini Mwanza, kulia Mwenyekiti wa Kongamano hilo, Somoe Nguhwe***

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Mhe. Amina Makilagi amesema Ushirika wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ukitumiwa na kuongozwa vizuri ni mkombozi wa uchumi kwa wanawake nchini.

Mhe. Makilagi amesema kupitia SACCOS mwanamke anaweza kufanya mambo mengi ya maendeleo kama atatumia mfumo mzuri wa kukopa na kurejesha. Ameeleza hayo oktoba 22, 2023 wakati wa Kongamano la Jukwaa la Wanawake wa SACCOS Kitaifa lililofanyika Jijini Mwanza.

Vile vile ametoa rai kwa wanawake kwenye SACCOS kuchangamkia fursa za kibiashara zinazotangazwa Serikalini kuomba na kuzifanya ili kuendelea kukuza mitaji katika Vyama vyao.

"Tenda za Serikali ni kwaajili ya watu wote, wanawake kwenye SACCOS changamkieni hizo fursa kwa kujiingiza katika biashara ili mitaji yenu iwe mikubwa muweze kukopa fedha nyingi kwa ajili ya kufanya mambo ya kimaendeleo," amesema.

Naye Mwenyekiti wa Kongamano hilo, Somoe Nguhwe, amesema wanaendelela kuhakikisha wanawake wanagombea nafasi za uongozi katika SACCOS zao. Nguhwe ameeleza kuwa SACCOS zinaongozwa na wanawake ndiyo ambazo zinaongoza kwa Hati Safi hii inaoesha wanawake wanafanya kazi nzuri na wanaweza zifikisha mbali SACCOS hizo.

## MRAJIS AFANYA MAZUNGUMZO NA MKURUGENZI MTENDAJI WA 'INTRACOM FERTILIZER LIMITED'



***Mrajis wa Vyama vya Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt.Benson Ndiege (katikati) akifanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda cha INTRACOM FERTILIZER LIMITED Nduwimana Nazaire (kushoto) Novemba 20,2023 Jijini Dodoma.***

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Mtendaji wa kiwanda cha 'INTRACOM FERTILIZER LIMITED', Nduwimana Nazaire, kuhusu namna bora Vyama vya Ushirika wa Mazao vinavyoweza kuwa wakala wa Mbolea ya RUZUKU inayotengenezwa Kiwandani hapo.

Mazungumzo hayo yamefanyika Novemba 20, 2023 Jijini Dodoma na kukubaliana Vyama Vikuu Vya Ushirika wa Mazao kwenda kuonana na Uongozi wa kiwanda hicho kujadiliana namna bora ya kuingia makubaliano hayo.



## WAKASUVI ATAKUMBUKWA DAIMA KATIKA KUSHIUGHULIKIA MAENDELEO NCHINI

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema Serikali itamkumbuka aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Tabora na mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Ndugu Hassan Wakasuvi kutokana na mchango wake mkubwa katika shughuli za maendeleo nchini.

Amesema hayo Februari 24, 2024 alipomwakilisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika maziko ya Ndugu Wakasuvi yaliyofanyika katika kijiji cha Mabama mkoani Tabora.

Amesema kuwa Ndugu Wakasuvi alikuwa kiongozi imara katika kusimamia shughuli za maendeleo ikiwemo sekta ushirika nchini na umahiri wake uliwezesha kuimarika kwa sekta hiyo na kuleta tija nchini. "Aliiwakilisha nchi vyema kwenye sekta ya ushirika sio Tanzania tu, bali Afrika Mashariki, Ndani ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Afrika kwa ujumla."

Akimwelezea Marehemu Wakasuvi, Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, amesemaTaifa limepoteza Mwalimu na Kiongozi aliyetoa mchango mkubwa katika sekta ya ushirika hapa nchini, Afrika na Dunia kwa ujumla ambaye alikuwa mdau muhimu wa maendeleo katika nyanja za Ushirika.

## MAADHIMISHO YA WIKI YA VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MKOPO - 2023 YAFANA



***Mkuu wa Wilaya ya Kwimba Mhe. Ng'wilabuzu Ludigija akifungua Maadhimisho ya Wiki ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo yaliyofanyika kitaifa Jijini Mwanza Oktoba 23, 2023***

Maadhimisho ya Wiki ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mkopo (ICUD) yaliyofanyika Kitaifa Jijini Mwanza Oktoba 23, 2023 yalifunguliwa na Mkuu wa Wilaya Kwimba, Mhe. Ng'wilabuzu Ludigija, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na kuwataka wanaushirika kuwa na mshikamano ili kuchangia katika maendeleo ya Taifa na kuunga mkono Kauli Mbiu ya mwaka huu, 'Wanachama Kusaidia Wanachama'.

Mheshimiwa Ludigija ameeleza kuwa Ushirika umeundwa mahsusi kuhakikisha kila mwanachama anashiriki kumsaidia mwanachama mwingine kwa njia ya kukusanya kwa pamoja rasilimali na kuzitoa kama huduma ili kulinda rasilimali hizi na kuhakikisha zinawanufaisha wengi.

Amevitaka Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) kuimarisha huduma zinazotolewa na kuweka udhibiti wa ndani, masharti na Sera huku wakifuata Sheria na taratibu zote ili kuufanya Ushirika uendelee kuwa huru na kujisimamia.



***Mtendaji Mkuu wa SCCULT Hassan Mnyone akimueleza jambo Mgeni Rasmi ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kwimba Mhe. Ng'wilabuzu Ludigija kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (ICUD) yaliyofanyika kitaifa Jijini Mwanza Oktoba 23,2023.***

"Hakikisheni mnajisimamia vema na maadhimisho haya yawe ni sehemu ya kujifunza na kupeana ujuzi, mkirudi katika maeneo yenu mzidi kuboresha Vyama vyenu pia endeleeni kufanya mambo yanayoigusa jamii moja kwa moja," amesema Ludigija

Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, amezitaka SACCOS kuendelea kuchangia kwa karibu kuimarika kwa mwamvuli wao (SCCULT) kwa kulipa Hisa, Michango ya mwaka pamoja na kuhakikisha wanawekeza kwenye Mfuko wa kukopesha SACCOS CFF uliopo SCCULT ili Mfuko huo uweze kuwanufaisha na kuzikopesha SACCOS wanachama zenye changamoto ya ukwasi.

## KONGAMANO LA SACCOS BARANI AFRIKA LAFANYIKA NCHINI BOTSWANA



***Mrajis wa Vyama vya Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt. Benson Ndiege, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa kifedha CPA Josephat Kisamalala na Viongozi wa Muungano wa SACCOS nchini (SCCULT) wakiwa kwenye picha ya pamoja na wenyeji wa Kongamano la SACCOS Africa lililofanyika nchini Botswana Oktoba***

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SCCULT) wameshiriki katika kongamano ambalo limeshirikisha nchi zaidi ya 30 kutoka mataifa mbalimbali lenye washiriki zaidi ya 700.

Kongamano hilo lililofunguliwa na Rais wa Botswana, Mhe. Mokgweetsi Masisi, limejadili masuala mbalimbali yanayohusu kuimarisha usimamizi, uendeshaji na utoaji wa huduma za SACCOS kwa wanachama.

Katika Kongamano hilo, wataalamu mbalimbali kutoka USA, Canada, Kenya, Uganda, Ghana, Tanzania, Afrika ya Kusini pamoja na mataifa mengine yalipata nafasi ya kufanya mawasilisho.

Kwa upande wa Tanzania, CPA Josephat Kisamalala, Mrajis Msaidizi anayesimamia Vyama vya Ushirika wa Kifedha alipata fursa ya kuwasilisha Mfumo wa Kisheria wa Usimamizi wa SACCOS Tanzania (SACCOS Regulatory Framework in Tanzania).

Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini Dkt. Benson Ndiege amefanya wasilisho Oktoba 13, 2023 ambapo alielezea namna mabadiliko ya Kisheria nchini yalivyosaidia kuwepo kwa mabadiliko ya uendeshaji, ukuaji na maendeleo kwenye Sekta ndogo ya SACCOS.

Katika kongamano hilo, Mrajis aliambatana na Naibu Mrajis anayesimamia Udhibiti, Collins Nyakunga, CPA Josephat Kisamalala, Mrajis Msaidizi anayesimamia Vyama vya Ushirika wa Kifedha, Mtendaji Mkuu wa SCCULT Hassan Mnyone pamoja na viongozi na watendaji wa SACCOS wapatao 50.

## WANACHAMA WA AMCOS WANUFAIKA NA MKOPO WA MATREKTA MANYARA

Wanachama sita wa Chama cha Msingi cha Ushirika, Mwamka AMCOS katika Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara wamekabidhiwa matrekta manne (4) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ikiwa ni mkopo wa awali wa matrekta sita (6) yatakayokopeshwa kwa Wakulima hao.

Mkopo huo wa matrekta una thamani ya jumla ya Shilingi Milioni 210 unaolenga kuwakopesha matrekta sita, ambapo matrekta manne yamekabidhiwa kwa Wanaushirika hao.



***Wanachama wa Mwamka AMCOS wakiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa AMCOS mara baada ya kukabidhiwa Trekta walizokopeshwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), makabidhiano yaliyofanyika Oktoba19, 2023 Wilaya ya Hanang Mkoani Manyara.***



## MRAJIS ATOA ONYO KWA VIONGOZI WA VYAMA WASIOFUATA SHERIA NA MIONGOZO YA USHIRIKA



***Mrajis wa Vyama vya Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt.Benson Ndiege akizungumza na Wanaushirika katika Kongamano la Vyama Vya Ushirika Wilaya ya Songwe Novemba 11, 2023.***

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, ametoa onyo kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika ambao bado wanaishi katika uongozi wa kijanja na kuacha kufuata miongozo na kanuni za Ushirika.

Mrajis ametoa onyo hilo Novemba 11, 2023 wakati wa kongamano la Vyama vya Ushirika Wilaya ya Songwe akimwakilisha Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussen Bashe, na kueleza kuwa Viongozi ambao watafanya kazi nzuri TCDC itawaunga mkono na ambaye atavuruga, Tume haitaweza kumvumilia. Hivyo, amewataka kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kusimamia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Aidha, amewataka wakulima wa Songwe kuendelea kujiunga katika Vyama vya Ushirika kwenye maeneo yao ili waweze kuwa na sauti ya umoja ambayo italeta maendeleo katika Vyama.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Mhe. Solomon Itunda, amesema kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la Ufuta, kumesababababisha ongezeko la mapato katika Wilaya hiyo kutoka kukusanya Shillingi Millioni 300 kwa mazao yote na kufikia Shillingi Millioni 800 kwa zao la Ufuta.



***Wanaushirika wa Vyama vya Ushirika wa Wilaya ya Songwe wakiwa kwenye Kongamano la Vyama Vya Ushirika lililofanyika Wilaya ya Songwe Novemba 11, 2023.***

Amesema mafanikio hayo si kwa Halmashauri tu hata kwa mtu mmoja mmoja wameweza kujipatia fedha nzuri kutokana na kuuza kwa kufuata Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwani wananchi wamepata mwitikio wa kuuza mazao yao kwa kufuata utaratibu.

Naye Kaimu Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Songwe (SORECO), Mon Mwampamba, amesema kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kumekuwa na ongezeko la ubora wa Ufuta na kupelekea ongezeko la bei za Ufuta kutoka Shilingi 1,700 ya awali hadi kufikia Shilingi 3,847 kwa kilo moja ya Ufuta hali hii imepelekea wananchi kuachana na uuzaji holela wa Ufuta.

## KCU NA NGARA FARMERS KUFANYA BIASHARA YA KAHAWA NA MAKAMPUNI YA JAPAN

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Kagera (KCU) Edson Rugaibamukamu, na Meneja wa NGARA FARMERS, Zephania Munyonyela, wamefanya ziara ya kikazi nchini Japan katika kutafuta masoko ya Kahawa ya wakulima badala ya Vyama hivyo kutegemea Madalali na Wanunuzi wa kati.



***Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Kagera (KCU) Edson Rugaibamukamu na Meneja wa Ngara Farmers Zephania Munyonyela wakiwa katika picha ya Pamoja na wenyeji wao walipofanya ziara ya kikazi nchini Japan***

Katika ziara hiyo wamefanikiwa kupata makampuni matatu makubwa watakayofanya nao biashara ya moja kwa moja. Aidha, Viongozi hao wa Ushirika wamefanikiwa kuonana na Balozi wa Tanzania Nchini Japani, Mhe. Baraka Luvanda na kumweleza mafanikio ya Ushirika nchini.

## CORECU LTD YAWALIPA SHILINGI BILIONI 8.8 WAKULIMA WA KOROSHO ZA MNADA WA KWANZA

Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU LTD), Hamisi Mantawela, amesema jumla ya Shilingi Bilioni 8.8 zimelipwa kwa wakulima wa Korosho wa mkoa huo.

Mantawela ameyasema hayo Novemba 15, 2023 kwenye Mnada wa Pili wa zao la Korosho uliofanyika katika wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Aidha, amesema kuwa jumla ya Tani 3,187 zilipelekwa sokoni na kampuni 10 zilijitokeza kuomba zabuni ya kuzinunua Korosho hizo.

Mantawela amewasisitiza Wakulima kuzingatia ubora wa zao la Korosho kwa kuwa bei bora zinatokana na ubora wa Korosho.

"Nichukue nafasi hii kuwaomba wakulima wetu kulinda ubora wa korosho zetu kwani tumeona hapa bei zimekuwa za kuridhisha hivyo tusiendelee kulewa sifa twendeni tukazianike korosho zetu ipasavyo huu ni mwanzo nzuri sana kwetu," amesema Mantawela



***Meneja Mkuu wa Chama cha Ushirika Mkoa wa Pwani, Hamis Mantawela, akizungumza na wanaushirika wakati wa mnada wa pili wa zao la Korosho uliofanyika Novemba 15, 2023 Wilayani Mkuranga - Pwani***

## DC MTWARA AVITAKA VYAMA VYA MSINGI KUHARAKISHA MALIPO KWA WAKULIMA WA KOROSHO

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Mhe. Mwanahamisi Munkunda, amevitaka vyama vya msingi kuharakisha malipo kwa wakulima wa Korosho kwa wakati, ili wananchi wapate fedha kwa ajili ya kununulia mahitaji mbalimbali ikiwemo chakula.

Mhe. Munkunda ameyasema hayo Novemba 11, 2023 kwenye Mnada wa nne uliosimamiwa na Chama Kikuu chu Ushirika MAMCU Ltd, uliofanyika Novemba 10, 2023.

"Wanunuzi walionunua Korosho wanaendelea kufanya malipo kupitia vyama vyao vya ushirika, niwaombe viongozi wa vyama kuharakisha malipo hayo yawafikie wakulima kwa wakati ili waweze kuendelea na shughuli zao zingie"

"Pia niwaombe tu wakulima kutumia vizuri malipo wanayoyapata ili yaweze kuwasaidia katika kufanya shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kupeleka watoto wao shule" amesisitiza Mkuu wa Wilaya.

Wakulima wa zao la Korosho katika Kijiji cha Mkahala Halmashauri ya mji wa Nanyamba mkoani Mtwara, wameuza kiasi cha zaidi ya Tani Elfu 6.5 za Korosho kwenye Mnada wa nne uliosimamiwa na Chama Kikuu chu Ushirika MAMCU Ltd.

Katika mnada huo, jumla ya Kampuni 30 zilijitokeza na kuwasiisha maombi ya kununua Korosho katika Maghala mbalimbali yaliyopo Masasi, Nanyumbu na Mtwara kwa bei ya juu ya Shilingi 2,000/= na bei ya chini shilingi 1,850/.



***Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Mhe. Mwanahamisi Munkunda akizungumza na Wanaushirika wa Vyama vya Ushirika wa Wilaya ya Mtwara kwenye mnada wa nne wa zao la korosho uliofanyika Novembaa 11, 2023 Wilayani Mtwara.***

## MNOLELA AMCOS - LINDI CHAKABIDHI MADAWATI SHULE YA SEKONDARI

Viongozi wa Chama cha Msingi Mnonela AMCOS wakikabidhi Madawati kwa Shule ya Sekondari Mnonela Novemba 08, 2023




***Chama cha Ushirika cha Msingi MNOLELA AMCOS kilichopo mkoani Lindi Novemba 08, 2023, kimekabidhi madawati 20 na viti 20 kwa Shule ya Sekondari Mnolela ikiwa ni kutekeleza Msingi wa Saba wa Vyama vya Ushirika katika kuijali jamii.***

## DC MTATIRO AVITAKA VYAMA VYA USHIRIKA KUTIMIZA MAJUKUMU YAKE KWA UAMINIFU NA UADILIFU



***Aliyejuwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Wakili Mhe. Julius Mtatiro akizungumza na Wanaushirika katika Ufunguzi wa minada ya zao la korosho uliofanyika Kata ya Nakapanya Wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Novemba 08, 2023***

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Mhe. Wakili Julius Mtatiro, amevisisitiza Vyama vya Ushirika nchini kuendelea kutimiza majukumu yake kwa uaminifu na uadilifu.

Ameyasema hayo katika ufunguzi wa minada ya zao la Korosho uliofanyika kata ya Nakapanya Wilayani Tunduru, ambapo aliwasisitiza watendaji wa Vyama vya Ushirika vya Msingi kufuata Miongozo, Sheria na Kanuni za Ushirika wanapotimiza majukumu yao.



***Wanaushirika wakiwa kwenye Ufunguzi wa minada ya zao la korosho uliofanyika Kata ya Nakapanya Wilayani Tunduru mkoani Ruvuma Novemba 08, 2023***

Aidha, Mhe. Mtatiro amesisitiza kuzingatia Usafi na Ubora wa Korosho zinazoingizwa ghalani, kwani ubora wa Korosho unasaidia kuongeza bei sokoni na hivyo kuleta tija kwa Mkulima.

## WAFANYABIASHARA WAENDELEA KUNUNUA HISA BENKI YA USHIRIKA



***Wakurugenzi wa Kampuni ya Umeme ya Tropical Cables ya Jijini Dar es salaam Aloyce Ngowi na Fedinard Mlawa wakiwa kwenye picha ya pamoja na Meneja Mkuu wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) Godfrey Ng'ura na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Dar es salaam Angela Nalimi kwenye zoezi la ununuzi wa hisa za KCBL.***

Wakurugenzi wa Kampuni ya Umeme ya Tropical Cables ya Jijini Dar es salaam ambao ni wafanyabiashara na wajasiliamali wenye mafanikio makubwa Aloyce Ngowi na Fedinard wachangia kiasi Shilingi za kitanzania Bilioni 4 ambayo ni sawa na asilimia 20 ya hisa za Benki ya Ushirika KCBL Oktoba 31, 2023 Jijini Dar es salaam.

Bodi na Menejimenti ya Benki ya Ushirika pamoja na Wanaushirika wamewapongeza Wafanyabiashara hao kwa uwekezaji mkubwa na wameahidi matokeo chanya na tija kwa uwekezaji huu wa kihistoria.

Viongozi waliohudhuria katika makabidhiano hayo ni pamoja na Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdul Majid Nsekela, Meneja Mkuu wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro, Godfrey Ng'ura, pamoja na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam, Anjela Nalimi.

## SACCOS ZATAKIWA KUJIUNGA NA SCCULT



***Katibu Tawala wa mkoa wa Mwanza Elikana Balandya akizungumza wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Vyama vya Akiba na Mikopo (ICUD) Oktoba26, 2023 Jijini Mwanza***

Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Elikana Balandya ametoa wito kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kujiunga na Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT) ili kuwa na uwakilishi wenye nguvu ambao upo imara na wenye kujiletea maendeleo.

Ametoa wito huo Oktoba 26, 2023 wakati wa kilele cha Maadhimisho ya wiki ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (ICUD) yaliyofanyika Jijini Mwanza.

Amesema kuwa viongozi wa SACCOS waendelee kutangaza masuala mazuri ambayo Ushirika wa Akiba na Mikopo umefanya kwa wanachama wake na shuhuda za kuaminika ndiyo utakuwa sehemu ya uhamasishaji ambao utaleta picha na mwonekano mzuri wa Ushirika wa Akiba na Mikopo.

Pia ameeleza ili SACCOS zizidi kuwa imara na zenye muelekeo mzuri wanachama wanapaswa kukopa na kulipa kwa wakati ili kuvipa nguvu vyama vyao na kuwapa wanachama wengine nafasi ya kupata huduma ya mikopo.

Akizungumza katika Maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Abdulmajid Nsekela, amesema kuendelea kuboresha SACCOS kutachangia kwa sehemu kubwa maendeleo na uchumi wa nchi. Hivyo, amewataka viongozi na wanachama waendelee kuungana katika

kuimarisha usimamizi wa shughuli za Vyama vyao.

Kwa upande wake Mrajis na Mtendaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, amesema kupitia SACCOS watu wamepata ajira 13,677 za kudumu na za muda mwaka 2022 ikilinganishwa na ajira 13,496 zilizokuwepo mwaka 2021.

Aidha, SACCOS zimeendelea kujali jamii kwa kutoa huduma mbalimbali za kijamii kwa kuzingatia msingi na 7 wa Vyama vya Ushirika wa kuijali jamii ambapo mwaka 2022 jumla ya watanzania 438,409 walipata Msaada kutoka kwenye SACCOS yenye thamani ya Shillingi Milioni 635.38.

## VIONGOZI SACCOS WATOA MSAADA KITUO CHA MAKAZI YA WAZEE BUKUMBI

kuelekea kilele cha Maadhimisho ya wiki ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mkopo (ICUD) Kitaifa Mkoani Mwanza baadhi ya viongozi wa Jukwaa la Wanawake na Viongozi wa SACCOS zilizoshiriki Maadhimisho hayo walitembelea kituo cha Makazi ya Wazee Bukumbi tarehe 25 Oktoba 2023 na kutoa msaada ikiwa ni moja ya malengo ya Jukwaa hilo katika kutekeleza msingi namba Saba wa Vyama vya Ushirika.



***Viongozi wa Jukwaa la Wanawake na Viongozi wa SACCOS wakiwa katika picha ya pamoja na Wazee wanaoishi katika Kituo cha Makazi ya Wazee Bukumbi Jijini Mwanza Oktoba25,2023.***

## MNADA WA TATU WA KOROSHO TUNDURU, KILO 6,140,450 ZIMEUZWA

Wakulima wa zao la Korosho wilayani Tunduru wameuza Korosho kilo 6,140,450 zilizoingia sokoni katika mnada wa tatu.

Mnada huo umefanyika Novemba 16, 2023 katika kijiji cha Angalia, Chama cha Msingi Mshikamano, ambapo wanunuzi 12 waliomba zabuni ya kununua kilo hizo 6,140,450.

Aidha, mahitaji kwa wanunuzi wote yalikuwa kilo 8,170,426 kwa bei ya Juu ya Shilingi 1,750 na bei ya chini 1,500 ambapo wanunuzi 5 pekee ndio walifanikiwa kushinda kununua korosho hizo kwa bei ya juu ya Shilingi 1,750 na chini 1,712 na kufanya bei wastani kuwa Shilingi 1,714.

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Ruvuma, Peja Muhoja, amewataka wasimamizi wa minada kutimiza majukumu yao kwa uaminifu na wakulima kuendelea kutunza ubora wa Korosho kwa kuzingatia hatua za kuandaa Korosho hadi hatua ya mwisho wanapozipeleka Ghalani kwani thamani ya Korosho inatokana na ubora wake.



***Wakulima wa zao la korosho wa Chama cha Msingi – Mshikamano wakiwa katika mnada wa tatu wa zao hilo uliofanyika Novemba 16, 2023 katika kijiji cha Angalia wilayani Tunduru mkoani Ruvuma.***

## MNADA WA KWANZA WA ZAO LA KOROSHO MKOANI LINDI

Mnada wa kwanza wa zao la Korosho mkoani Lindi Oktoba 21, 2023 uliofanywa na Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao, ambapo wakulima walikubali kuuza Korosho zao kwa bei ya juu Shilingi 2,032/= na bei ya chini Shilingi 1,965/. Mahitaji yalikuwa Kilo 18,700,953.



***Viongozi wa Vyama vya Ushirka wakiwa katika mnada wa kwanza wa zao la korosho uliofanyika katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Lindi Mwambao Oktoba21, 2023***



***Wakulima wa zao la korosho wakiwa katika mnada wa kwanza wa zao la korosho uliofanyika katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Lindi Mwambao Oktoba 21,2023***

## HAKIKISHENI VIPAUMBELE VYA TUME VINATEKELEZWA – MRAJIS



***Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) Dkt. Benson Ndiege akizungumza na Watumishi wa TCDC kwenye kikao cha tatu cha Watumishi wote kilichofanyika mkoani Dodoma.***

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amewataka Watumishi wa TCDC na watendaji wa Vyama vya Ushirika kutekeleza vipaumbele vya saba (7) vya Tume kama vilivyotolewa na Kamisheni ya Tume ili kuleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Ushirika.

"Hakikisheni mnavijua na kuvitekeleza Vipaumbele saba (7) vya Tume na kuvifanyia kazi ipasavyo kama vilivyotolewa na Kamisheni ya Tume", amesema Dkt. Ndiege.

Mrajis ameyasema hayo Disemba 22, 2023 Jijini Dodoma katika Kikao cha tatu (3) cha Watumishi wote wa Tume wa Makao Makuu na Wawakilishi wa mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.



***Godamen Merinyo Afisa Ushirika kutoka mkoa wa Manyara, akichangia wakati wa kikao cha Watumishi wa TCDC kilichofanyika Jijini Dodoma.***

Dkt. Ndiege amevitaja Vipaumbele hivyo kuwa ni Uwekezaji katika Mifumo ya kisasa ya kidigitali; Kurahisisha Mchakato wa uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika; kuhamasisha Mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara; Kuboresha Sera; Sheria na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika; Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na makundi maalumu; Kuimarisha uwekezaji na Mali za Ushirika katika uzalishaji; na Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza Sekta Ushirika.

Aidha, amesisitiza kuwa katika kutekeleza vipaumbele hivyo, viongozi wasiruhusu Watu kuchezea na kuharibu Mifumo ya Ushirika.

"Msiruhusu watu wachezee mifumo ya Ushirika (ikiwemo Mfumo wa MUVU) msiruhusu watu waharibu, nami katika hilo nitawaongezea nguvu," amesema Dkt. Ndiege.

Mrajis pia amewataka Watumishi kuwa waadilifu katika utendaji wa kazi na kutumia vizuri fedha zinazopelekwa kwa ajili ya Usimamizi wa Vyama ili kuleta mabadiliko chanya ya kisekta na Taifa kwa ujumla.

"Pamoja na mengine, tuna changamoto ya uaminifu, hili lazima tubadilike, hatuna nia ya kumuumiza mtu, tunahitaji uadilifu na jitahidini kuwa waadilifu katika

kusimamia Vyama," amesema Mrajis.

## TUMAINI SACCOS CHAFANYA MKUTANO MKUU WA 34

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Tumaini SACCOS Ltd kimefanya Mkutano Mkuu wa 34 Oktoba 21, 2023 Jijini Arusha ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Collins Nyakunga.

Naibu Mrajis amewataka Viongozi wa Vyama vya Ushirika kuwa waaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao na amewataka wanachama wa SACCOS kuwa waaminifu katika urejeshaji wa mikopo yao kulingana na makubaliano waliyoingia.



***Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika (Udhibiti) Collins Nyakunga akiongea na Viongozi na Watendaji wa Tumaini SACCOS LTD kwenye Mkutano Mkuu wa 34 wa SACCOS hiyo uliofanyika Oktoba21, 2023 Jijini Arusha.***



***Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika (Udhibiti) Collins Nyakunga akiwa kwenye picha ya pamoja na Viongozi na Watendaji wa Tumaini SACCOS LTD kwenye Mkutano Mkuu wa 34 wa SACCOS hiyo uliofanyika Oktoba 21, 2023 Jijini Arusha.***

## VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA WATAKIWA KUACHA KUTANGULIZA MASLAHI BINAFSI

Wanaushirika wanaogombea na kupata nafasi za uongozi katika Vyama vya Ushirika wametakiwa kuacha kutanguliza mbele maslahi binafsi mara wanapochaguliwa katika nafasi za Uongozi.

Kauli hiyo imetolewa Jijini Dar es Salaam hivi karibuni na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Morogoro Kenneth Shemdoe, alipokuwa akisimamia uchaguzi wa Bodi Mpya na Kamati ya Usimamizi katika chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo - Women Advancement TRUST (WAT SACCOS) cha Jijini Dar es Salaam ulofanyika tarehe 14 Oktoba, 2023 katika ukumbi wa NGOME Holding, Sinza.



***Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Morogoro, Kenneth Shemdoe, akizungumza alipokuwa akisimamia Uchaguzi wa Bodi wa Bodi Mpya na Kamati ya Usimamizi katika Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo – WAT SACCOS uliofanyika Oktoba 14, 2023 Jijini Dar es salaam.***

"Ni marufuku Mwanaushirika anayetaka na baadae kuupata uongozi wa kuchaguliwa katika chama cha Ushirika na sekta nzima ya Ushirika kutafuta madaraka na kuyapata huku akiwa na ajenda yake mfukoni. Ajenda ya kukitumia chama cha Ushirika kwa manufaa binafsi," alionya Shemdoe ambaye alisimamia uchaguzi huo Kwa niaba ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika uchaguzi wa Bodi ya Uongozi ya WAT SACCOS, wajumbe tisa walichaguliwa kuingia katika Bodi

huku Bazil Kimario na Helen Ngoto wakichaguliwa kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bodi mtawalia.

Wajumbe wengine wa Bodi waliochaguliwa ni Beatrice Assenga, Saada Kiponza, Mary Kakila, Cyprianus Kunkuta, Prosper Haule, Saida Mukhi na Lugenzi Kabale.

## WANAUSHIRIKA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MBOLEA DUNIANI




**Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Tabora Venancy Msafiri akizungumza wakati alipotembelea banda la TCDC kwenye maadhimisho ya Wiki ya Mbolea Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Tabora Okoba 11 – 13,2023**

Kufuatia ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani ambayo kitaifa yamefanyika Mkoani Tabora, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imebainisha mchango wa Wanaushirika katika maendeleo ya Kilimo ambao wanabeba idadi kubwa ya Wakulima wanaofaidika na mbolea.

Akizungumza kwa niaba ya Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Tabora, Venance Msafiri, ameeleza kuwa, TCDC ina majukumu makubwa mawili ambayo inayatekeleza kupitia vyama vya msingi ambavyo vinajumuisha idadi kubwa ya wakulima ambao hufaidika na mbolea moja kwa moja.

"Tume ina majukumu makubwa mawili, kwanza ni usimamizi na udhibiti wa vyama vya Ushirika na pili ni kufanya uhamasishaji kwenye vyama vya Ushirika na sehemu zote za kiuchumi," amesema Mrajis Msaidizi.

Sambamba na hilo, Msafiri amebainisha umuhimu wa Maadhimisho ya Siku ya Mbolea kwa wakulima ambao mpaka sasa idadi yake ni kubwa na wanafaidika kwa kiasi kikubwa na maadhimisho haya ambayo wakulima wanapata fursa ya kujifunza mambo kadha wa kadha kuhusu mbolea.

"Nchi nzima kuna vyama vya Ushirika zaidi 7,300 ambavyo vina jumla ya wanachama zaidi ya 8,000,000, ambapo AMCOS zipo 4,252 na zina wanachama zaidi ya 5,000 ambao kwenye maadhimisho haya wanashiriki, na idadi kubwa ya wanachama ni wakulima na wanatumia mbolea," amesisitiza Msafiri.

Maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yamefanyika Mkoani Tabora kuanzia Oktoba 11, 2023 hadi Oktoba 13, 2023, yenye Kauli mbiu isemayo "AGENDA 10/30: Matumizi Sahihi ya Mbolea ya Ruzuku kwa Kilimo Chenye Tija"

## AMCOS TABORA ZAMPONGEZA NA KUMSHUKURU RAIS DKT. SAMIA

Zaidi ya wanachama 420 kutoka vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) Mkoani Tabora wamempongeza na kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha wakulima wa Tumbaku wanapata Mbolea ya Ruzuku ya kutosha na kwa wakati pasipo na changamoto zozote kama ilivyokuwa hapo awali.

Hayo yamejiri Oktoba 6, 2023 wakati wa Ufungaji wa Mafunzo ya Wenyeviti na Watendaji wa AMCOS zilizopo Wilayani Urambo na Kaliua uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Balozi Batilda Burian.



***Aliyekuwa Mkuu wa mkoa wa Tabora Mhe. Balozi Batilda Buriani akifunga Mafunzo ya Wenyeviti na Watendaji wa AMCOS zilizopo Wilayani Urambo mkoani Tabora Oktoba 06, 2023.***



**Wenyeviti na Watendaji wa AMCOS zilizopo Wilayani Urambo mkoani Tabora wakiwa kwenye Mafunzo ya Utendaji kazi yaliyofanyika Oktoba 06, 2023.**

## MAMCU YAWALIPA WAKULIMA WA KOROSHO SHILINGI BILIONI 81 KATIKA MINADA MINNE MSIMU HUU

Chama Kikuu cha Ushirika wilaya ya Mtwara, Masasi na Nanyumbu (MAMCU Limited) kimewalipa wakulima wa Korosho kiasi Shilingi Bil. 81 katika minada minne iliyofanyika tangu kuanza kwa msimu wa mwaka 2023/2024.

Akizungumza katika kata ya Kilimahewa, Wilayani Nanyumbu Novemba 17, 2023 ulikofanyika mnada wa tano wa zao hilo, Meneja Mkuu wa chama hicho, Biadia Matipa, amesema kuwa malipo hayo ni kutokana na mauzo ya Korosho tani 41, 042.



***Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Mtwara, Masasi na Nanyumbu (MAMCU Ltd) Biadia Matipa akizungumza na Wanaushirika kwenye mnada wa tano wa Korosho uliofanyika Novemba 17,2023 katika Kata ya Kilimahewa Wilayani Nanyumbu Mkoani Mtwara.***



***Wanaushirika wakiwa kwenye mnada wa tano wa Korosho uliofanyika Novemba 17,2023 katika Kata ya Kilimahewa Wilayani Nanyumbu Mkoani Mtwara.***

Amefafanua kuwa katika mnada wa kwanza wameuza Korosho tani 9,835 zenye thamani ya Shilingi 19,183,580,521 na mnada wa pili zimeuzwa korosho tani 12,222 zenye thamani ya Shilingi 24,236,042,781.

Aidha, katika mnada wa tatu wameuza Korosho tani 10,414 zenye thamani ya Shilingi 21,252,742,463, huku mnada wa nne zikiuzwa Korosho tani 8,570 zenye thamani ya Shilingi 16, 355,245,194.

Meneja ameongeza kuwa katika mnada wa tano jumla ya kampuni 32 zimejitokeza kununua Korosho tani 12,773 ambazo zimepelekwa sokoni na bei zilizojitokeza ni bei ya juu ya shilingi 1,855 na ya chini 1,700.

## NG'AMBO SACCOS YATOA MSAADA KWA KITUO CHA WAZEE WASIOJIWEZA CHA NJORO, MOSHI



***Viongozi wa Ng'ambo SACCOS LTD wakiwa kwenye picha ya pamoja na Wazee wa Kituo cha Wazee Njiro walipokwenda kutoa msaada katika kituo hicho Disemba 13, 2024.***

Katika kutekeleza Msingi wa Ushirika wa Kuijali Jamii, Desemba 13, 2023 Ng'ambo SACCOS LTD imetimiza msingi huo kwa watendaji na Wajumbe wa Bodi kuwatembelea na kuwapelekea wazee wa kituo cha Wazee wasiojiweza cha Njoro mahitaji mbalimbali ya kujikimu.

Mahitaji yaliyowasilishwa ni pamoja na vyakula, **vifaa**

vya usafi na madawa.

Viongozi wa Ng'ambo SACCOS wameushukuru uongozi na watumishi wa kituo hicho kwa kuwapokea na kuwapa ushirikiano mzuri kwenye kutimiza azma yao.

"Zaidi sana sote tuliofika kituoni tumebarikiwa sana kuwaona wazee tukakaa nao na kuwaombea Mungu awape utulivu wa changamoto za kuugua na uzee; wazee wamefurahi sana kwa uwepo wetu kituoni na kwa misaada tuliyowapelekea na kutuombea Baraka tele za kutoka kwa Mungu wetu," wamesema.

## CHAMA CHA USHIRIKA KUPATIWA MKOPO NA TADB KUIMARISHA UFUGAJI WA SAMAKI

Chama cha Msingi cha Ushirika cha 'Lake Multipurpose Primary Cooperative Society Limited' cha Wilayani Magu katika Mkoa wa Mwanza kimeingia mkataba na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwaajili ya kupatiwa mkopo wa jumla ya Shilingi 117,502,683.71.



***Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mohamed Kyande (katikati), na Afisa Ushirika Mkuu wa Ofisi za TCDC Wilaya ya Magu, Richard Majala (wapili kushoto).***

Madhumuni ya mkopo huo ni ununuzi na ufungaji vizimba vya kufugia samaki, ununuzi wa vifaranga vya samaki, ununuzi wa chakula cha samaki na bima ya mradi (Vizimba na Vifaranga) ya mwaka mmoja. Mkopo huo utakuwa wa miaka mitano huku mwaka wa kwanza ukiwa kipindi cha msamaha (grace period).

Mkataba huo uliotiwa saini Jumanne ya tarehe 12 Disemba 2023, ikiwa ni sehemu ya utekelezwaji wa Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) ili kunufaika na fursa zitokanazo na utekelezwaji wa dhana ya Uchumi wa Bluu. Serikali imetenga fedha mahsusi, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa malengo ya kukopesha wadau mbalimbali, vikiwemo vyama vya ushirika, vinavyoojishughulisha na ukuzaji na uendelezwaji wa viumbe hai wa majini.

Utiwaji saini wa mkataba huo umefanyika katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Magu na kushuhudiwa na Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mohamed Kyande, na Afisa Ushirika Mkuu wa Ofisi za TCDC Wilaya ya Magu, Richard Majala.

## RAMADHAN MIRAJI MWENYEKITI MPYA TCDC SACCOS



***Mwenyekiti wa TCDC SACCOS Ramadhan Miraji mara baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika katika mkutano wa Saba (7) wa chama hicho Disemba 08, 2023.***

Mkutano Mkuu wa Saba (7) wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo TCDC (TCDC SACCOS LTD) umefanyika tarehe 08/12/2023 kwenye ukumbi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Makao makuu Dodoma, ambapo jumla ya wanachama 62 walihudhuria.

Katika Mkutano Mkuu huo, Wanachama walifanya uchaguzi wa wajumbe wa Bodi wapya wa Chama na Kamati ya Usimamizi. Wajumbe wa Bodi waliochaguliwa ni Ramadhan Miraji (Mwenyekiti), Flora Daud (Makamu Mwenyekiti), Ndimolwo Laizer, Revocatus Nyagilo na Beatrice Mwanjala; na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ni Ntambi Bunyazu, Grace Mwengende na Colletha Bilabaye.

Mkutano Mkuu huo ulijikita katika kujadili mafanikio na maendeleo ya Chama kwa mwaka uliopita na mwelekeo wa Chama kwa mwaka mpya wa 2024.

Aidha, kupitia mijadala ya wanachama na wajumbe waliohudhiria, wameazimia kila mwanachama kukamilisha mafungu yote ya hisa kama ilivyo kwa mujibu wa Masharti ya Chama.



***Makamu Mwenyekiti wa TCDC SACCOS Flora Daud mara baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo katika uchaguzi uliofanyika katika mkutano wa Saba (7) wa chama hicho Disemba 08, 2023.***

Viongozi waliochaguliwa kufanya kazi kwa weledi ili kufanya Chama kupiga hatua zaidi kutoka hapo ilipo katika nyanja ya Uchumi na kujibu mahitaji ya waanzilishi wake.

Wanachama wameazimia kutanua wigo wa uwekezaji kwa kuongeza vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo uanzishaji wa huduma zingine za kifedha ikiwemo uwakala wa mitandao ya simu na benki.

Aidha, Wanachama wote wametakiwa kufikisha Akiba kiasi kisichopungua Milioni 2 kama ilivyo kwa mujibu wa Masharti ya Chama.



# JENGO LA OFISI YA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA LINDI MWAMBAO LILILOGHARIMU SHILINGI 416,904,460 LAZINDULIWA



***Mrajis wa Vyama vya Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt. Benson Ndiege (katikati) akizindua Jengo la Ofisi za Chama Kikuu cha Lindimwambao Disemba 07, 2023.***

Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, amezindua jengo la Ofisi ya Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao lililogharimu shiling 416,904,460 ikiwa ni mapato ya ndani ya Chama hicho ikiwa ni gharama ya jengo na uzio wake.

Jengo hilo limezinduliwa tarehe 07 Desemba, 2023 ambapo Mrajis amesema Chama hicho kimeonesha mfano mzuri kwenye Vyama vya Ushirika kwa kuweza kujenga Ofisi ya kisasa kwa kutumia mapato yake ya ndani ambayo itaongeza ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

“Naimani kupitia mradi huu wa Ofisi yenu ya kisasa na sasa ikawe chachu kwa Vyama vingine vya Ushirika kuweza kujenga Ofisi zao. Pia nawaasa kutunza vizuri jengo hii ili liweze kudumu kwa muda mrefu na jengo linahitaji mambo ya kidigitali tumieni sana mifumo katika kufanya kazi zenu,” amesema Dkt. Ndiege

Mrajis mesema pamoja na maendeleo yanayofanywa na Chama Kikuu, vipo Vyama vya Msingi vimeweza kuanzisha miradi ya maendeleo kwa kujenga miundombinu mbalimbali kama ghala, ofisi na nyumba za kulala wageni na Vyama vingine vimeweza kununua malori na wanasafirisha mazao yao wenyewe kuyapeleka kwenye ghala na hivi ndiyo tunavyotaka Ushirika uwe.

Meneja Mkuu cha Chama cha Lindi Mwambao, Nurdin Swala, amesema ujenzi wa Ofisi yao ulifuata taratibu zote na kuridhiwa na Bodi na wanachama. Ujenzi huo ulianza rasmi mwezi Machi 2022 na kukamilika Agosti 2023.

Swala amesema jengo hilo litasaidia kuongeza tija kwa kuwahudumia wanachama na wadau wengine na kuongeza ufanisi wa kazi kwa watendaji na usimamizi wa Bodi kwasababu mazingira ya jengo ni rafiki kwa kufanyia kazi.

## 'COOP MOBILE BANKING' YA BENKI YA USHIRIKA KILIMANJARO YAZINDULIWA

Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) imezindua bidhaa mpya ya Kidigitali ya 'COOP MOBILE BANKING' Disemba 6, 2023.

Bidha hii inamuwezesha mteja wa KCBL kupata huduma za kifedha kupitia simu yake ya Kiganjani kama vile kuangalia salio, taarifa za akaunti, kuhamisha fedha, kununua LUKU, kulipa bili na kufanya malipo ya Serikali (GePG).




***Meneja Mkuu wa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) Godfrey Ng'ura akiwa kwenye picha ya pamoja na Viongozi wengine wa ushirika katika uzinduzi wa bidhaa mpya ya kidigitali ya 'Coop Mobile Banking' uliofanyika Disemba 06, 2023***

Aidha, bidhaa hii inapatikana kupitia USSD *150*84# na APP (Google Play store na Apple Store).

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo Boma Raballa, Afisa Msimamizi Mkuu wa Biashara, Benki ya CRDB.

## SHAMBA LA HEKARI 1,600 LA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA MAMCU LTD LAZINDULIWA

Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, ametembelea na kuzindua shamba la Chama Kikuu cha Ushirika Masasi na Mtwara MAMCU LTD lenye hekari 1,600.

Akizindua shamba hilo tarehe 06 Desemba, 2023 kijiji Ndechela cha Wilayani Nanyumbu amesema Bodi ya chama ni jukumu lao kuhakikisha shamba hilo linakuwa na hati pamoja na mipaka itakayosaidia kuepusha wavamizi katika eneo hilo.



***Mrajis wa Vyama vya Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt.Benson Ndiege (katikati) akizindua shamba la hekari 1,600 la Chama kikiuu cha MAMCU LTD Disemba 07,2023***

Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, ametembelea na kuzindua shamba la Chama Kikuu cha Ushirika Masasi na Mtwara MAMCU LTD lenye hekari 1,600.

Akizindua shamba hilo tarehe 06 Disemba, 2023 kijiji Ndechela cha Wilayani Nanyumbu amesema Bodi ya chama ni jukumu lao kuhakikisha shamba hilo linakuwa na hati pamoja na mipaka itakayosaidia kuepusha wavamizi katika eneo hilo.

Vilevile ametoa rai kwa Bodi hiyo kusimamia mradi huo kwa weledi, kuhakikisha unakamilika kama ambavyo wamekubaliana katika vikao vyao na kusimamia ulipaji wa deni walilokopa kwa ajili ya shamba hilo linalipwa kwa wakati.

"Mkisimamia hili shamba kwa uaminifu na weledi naimani kabisa hili deni mnaweza kulilipa kwa kulima Mbaazi na Ufuta lipeni mpate fursa ya kukopa tena ili muendele kuwa na miradi ya Chama," amesema Dkt. Ndiege.

Kwa upande wake Meneja Mkuu wa MAMCU, Biadia Matipa, amesema waliamua kununua shamba hilo ili waweze kulima kilimo cha mkakati na kufikia kulima

tani 700 kwa mbaazi ifikapo 2025.

Biadia amesema shamba hilo likianza litaleta mafanikio kama kutoa ajira mbalimbali pia litaongeza kipato cha Chama na kuepuka kuwa wategemezi wa ushuru na litafanya ongezeko la Mali za kudumu za Chama hicho.

## NAIBU WAZIRI AZINDUA MATUMIZI YA MIZANI ZA KIDIGITALI ZILIZOUNGANISHWA NA MFUMO 'MUVU'



***Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde akizindua Matumizi ya Mizani ya Kidigitali uliounganishwa na MUVU wilayani Tandahimba mkoani Mtwara Disemba 05,2023***

Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Mhe. David Silinde (Mb) amezindua matumizi ya Mizani za Kidigitali zilizounganishwa na Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) utakaoimarisha utendaji na uendeshwaji wa Vyama vya Ushirika nchini.

Mhe. Silinde amesema sasa ni zama za Kidijitali hivyo Vyama vyote vya Ushirika wa Mazao nchini vitumie Mizani ya Kidijitali iliyounganishwa na Mfumo wa upimaji wa Mazao katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Silinde ameeleza hayo tarehe 5 Disemba, 2023 Wilaya ya Tandahimba Mkoani Mtwara alipokuwa akizindua mizani hizo na kugawa mbegu za Mbaazi kwa wakulima wa Wilaya ya Tandahimba.

Amesema baada ya uzinduzi ni kusimamia na kuhakikisha Viongozi na Watendaji wote wa Vyama vya Ushirika wanasimamia matumizi sahihi ya Vipimo pamoja na matumizi ya Mizani ya Kidijitali iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo nchini.

Kwa upande wake Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amesema Mkoa wa Mtwara una Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) 726 ambavyo vinavyojishughulisha na mazao ya Korosho, Ufuta na Mbaazi pamoja na vituo vyake vya kukusanyia vipatavyo 2,236 inahitajika vituo vyote hivyo kutumia Mfumo wa Upimaji wa Mazao ya Wakulima ulioounganishwa na mizani za kidijitali.

Dkt. Ndiege ameeleza kuwa, wanatarajia kusambaza kompyuta mpakato (Laptop) 726 kwa AMCOS zote zitakazofikishiwa Mizani kwa lengo la kuwezesha na kurahisisha utendaji kazi hususan katika kuwahudumia wakulima.

Amesema matarajio ya Serikali kuhusu matumizi ya Mifumo hii iliyounganishwa na Mizani ya Kidijitali, kwa kiwango kikubwa ni kusaidia kupunguza malalamiko ya wakulima kupunjwa kilo za mazao yao na kuwezesha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi kwa wakati.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ushirika wa Mradi wa Pamoja wa Korosho Ltd, Odas Mpunga, amesema mizani hizo zitasaidia kutatua changamoto kwa wakulima na amemuhakikishia Naibu Waziri kuwa watasimamia vyema na kwa uadilifu mkubwa mizani hizo kwa masilahi ya wakulima wanaowahudumia.

## NAIBU WAZIRI SILINDE AWATAKA VIONGOZI WA USHIRIKA KUFANYA KAZI KWA UADILIFU NA UAMINIFU

Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde, amewataka Viongozi wa Vyama vya Ushirika na Maafisa Ushirika kufanya kazi kwaweledi, uadilifu na uaminifu.

Amesema Viongozi wa Vyama na Maafisa Ushirika wakifanya kazi kwa uadilifu itasaidia kujenga imani kwa Wanaushirika na kuongeza idadi ya wanachama katika maeneo yao.



***Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde akizungumza na Viongozi wa Vyama vya Ushirika wakati akipokea taarifa ya Ushirika kwa mkoa wa Lindi Disemba 04, 2023.***

Mheshimiwa Silinde ameeleza hayo tarehe 4 Desemba, 2023 wakati akipokea taarifa ya Ushirika katika Mkoa wa Lindi.



***Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. David Silinde akizungumza na Viongozi wa Vyama vya Ushirika wakati akipokea taarifa ya Ushirika kwa mkoa wa Lindi Disemba 04, 2023.***

Aidha, amesema ni wajibu wa Vyama na Maafisa Ushirika kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo yao ili kuongeza idadi ya wanachama na kuwaunganisha wanachama na si kuwatenganisha.

Naye Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amesema wajibu wa Vyama ni kutengeneza mazingira rahisi ambayo yatarahisisha na kufanya wakulima kujiunga kwa hiari katika Vyama wanavyopeleka mazao yao.

"Wote mnajua kuwa mtu kujiunga na Ushirika ni hiari ila ni wajibu wenu kufanya mambo ambayo yatamvuta Mkulima na kuamua kujiunga na Ushirika kwasababu ndiyo sehemu salama kwa Mkulima," amesema Dkt. Ndiege.

## MAMCU YACHANGIA MILIONI 75 KWA WILAYA ZA MASASI, MTWARA NA NANYUMBU KUSAIDIA UJENZI WA MADARASA



***Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika MAMCU LTD Siraji Mtenguka akizumza katika uzinduzi wa Bonanza la Walimu wa shule zilizopo Halmshauri ya Wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba Disemba 03,2023***

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU LTD), Siraji Mtenguka, amesema kuwa chama chake kimetoa jumla ya Shilingi 75 milioni kwa wilaya tatu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.



***Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika MAMCU LTD Siraji Mtenguka akikata utepe katika uzinduzi wa Bonanza la Walimu wa shule zilizopo Halmshauri ya Wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba Disemba 03,2023***

Amesema hayo Desemba 3, 2023 katika uzinduzi wa Bonanza la walimu wa shule zilizopo katika Halmashauri ya wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya mji Nanyamba.

Mtenguka amesema wameona kuwekeza nguvu katika sekta za afya, elimu, maji na miundombinu ambapo kwa ujumla wake wameshatoa jumla Shilingi 203 Milioni kuhudumia wananchi katika sekta hizo za kijamii.

"Tumewekeza nguvu zetu katika sekta ya elimu ili kumkomboa Mtanzania ambaye ni mtoto wa mwanaushirika mwenzetu kwani kwa kufanya hivi itasaidia jamii yetu inayotuzunguka kupata elimu bora," amesema Mtenguka.

## TCDC KUSIMAMIA IPASAVYO MKATABA KATI YA VYAMA VYA USHIRIKA NA KIWANDA CHA MBOLEA CHA INTRACOM



***Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) Dkt.***

***Benson Ndiege alipotembelea kiwanda cha Intracom Fertilizer Ltd Novemba 30, 2023 Jijini Dodoma***

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amemhakikishia Mkurugenzi wa kiwanda cha mbolea cha INTRACOM kuwa mikataba itakayoingiwa na Vyama Vya Ushirika na Kiwanda hicho itasimamiwa ipasavyo na TCDC.

"Nikutoe hofu na nikuhakikishe tutafanya kazi nzuri kwasababu hakutokuwa na Risk ya kupoteza chochote katika makubaliano yetu kwasababu tunaingia mkataba na Chama na si mtu mmoja mmoja," amesema Dkt. Ndiege.

Ametoa kauli hiyo tarehe 30 Novemba, 2023 wakati wa kikao na Viogozi wa Vyama Ushirika vya MBIFACU LTD, CHUTCU LTD, TANECU LTD, KACU LTD, SORECU LTD, CORECU LTD, KDCU LTD, WETCU LTD, WAMACU LTD, LINDI MWAMBAO, RUNALI, NGARA FARMES, IFCU LTD, UFIPA CU LTD, TAMCU LTD, TANCCOOPS LTD na TFC kiluchofanyika katika Kiwanda cha Mbolea cha INTRACOM FERTILIZER LIMITED.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mbolea INTRACOM FERTILIZER LIMITED, Nduwimana Nazaire, amevialika Vyama Vya Ushirika kujadili namna ya kuanza kufanya kazi na Vyama hivyo kwa kuwa Wakala wa mbolea ya Fomi na kuisambaza kwa wakulima wanaowahudumia.

Nazaire amesema hakuna kitakachoshindikana katika makubaliano yatakayofikiwa kwa lengo la kufanya biashara ambayo ni endelevu na kueleza amefurahishwa na ugeni huo kiwandani hapo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa TANCCOOPS LTD, Zainabu Mahenge, amesema anaushukuru uongozi wa TCDC kwa kuwatafutia fursa hiyo ambayo itawafanya waweze kuwahudumia vizuri wanachama wao katika suala la mbolea na kuomba INTRACOM kuwaamini ili waweze kufanya biashara.



## WANUNUZI WA KAHAWA AINA YA 'ORGANIC' WATEMBELEA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA KCU



***Wanunuzi wa Kahawa ya Organic kutoka nchini Ujerumani wakiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika (KCU) Novemba 28, 2024 mkoani Kagera.***

Chama Kikuu cha Ushirika KCU kilichopo mkoani Kagera tarehe 28 Novemba 2023 kimetembelewa na Wanunuzi wa Kahawa aina ya 'Organic' toka nchini Ujerumani.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya mnunuzi na mzalishaji, kwenye Soko la Haki (Fair Trade) ili mnunuzi ajue changamoto za uzalishaji kwa lengo la kuboresha bei ya mkulima.

Katika ziara hiyo Wanunuzi wameweza kuongea na wanachama wa Bujugo AMCOS na kutembelea Ghala kubwa la Kemondo linalohifadhi Kahawa ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi kwa wanunuzi.

Ushirikiano huo umeweza kuleta mradi wa majiko sanifu kwa wakinamama wanachama wa Vyama vya Ushirika vya msingi 45 vilivyopo kwenye Mradi wa 'Organic Coffee'.

## MAKAMISHNA WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA WATEMBELEA VITEGA UCHUMI VYA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA NYANZA



***Makamishna wa TCDC pamoja na Naibu Mrajis (Udhibiti) wakiwa kwenye ziara katika vitega uchumi vya Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza (NCU) Novemba 28, 2024 Jijini Mwanza***

Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), wamefanya ziara ya kutembelea vitega uchumi vya Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza (NCU) ikiwemo Majengo na Hosteli zilizopo katikati ya Jiji la Mwanza na eneo la KAUMA kwenye jengo na ghala la kukodi pamoja na kituo cha mafuta.

Vilevile, Makamishna wametembelea kiwanda cha kuchambua Pamba kilichopo eneo la Manawa wilayani Misungwi.

"Hiki kiwanda cha kuchambua Pamba kiliundwa mwaka 1990 na kilichangia sana maendeleo ya zao la Pamba kwani mikoa 7 ya Kanda hii ya Ziwa na jirani ilikuwa inaleta Pamba na kuchambuliwa kabla ya kukifunga mwaka 2014; tumeomba fedha Serikalini Shilingi milioni 800 ili tuweze kukifufua," amesema Elisha Midamo, Meneja Uzalishaji wa NCU.

Kamishna Richard Mayongela amekishauri chama hicho kukutana na uongozi wa Benki mbalimbali ili uweze kupata mkopo wenye riba nafuu kupitia mali ilizonazo zenye thamani kubwa.

"Ziara yetu ya siku mbili tukiwa hapa Mwanza tutahimiza sana chama hiki kiwe na wingi wa wanachama wake ambao ndiyo mtaji wa kuwa na nguvu pia kitumie vizuri fursa za mali zake kujiongezea kipato," amesema Mayongela.

Viongozi hao wamehitimisha ziara hiyo Novemba 28, 2023 kwa kuzitembelea baadhi ya Saccos zilizopo Wilaya za Nyamagana, Ilemela na Magu.

## KACU NA SHIRECU WASHIRIKI 'SHINYANGA BUSINESS FORUM' KUTANGAZA 'USHIRIKA NI BIASHARA'




***Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Shinyanga Hilda Boniface (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Viongozi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Shinyanga katika maonesho ya Kibiashara yaliyoandaliwa na TCCIA yaliyofanyika mkoani Shinyanga***

Vyama Vikuu vya Ushirika Mkoa wa Shinyanga (KACU LTD na SHIRECU LTD) vimeshiriki Katika Maonesho ya Biashara ('Shinyanga Business Forum) yaliyoandaliwa na TCCIA kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkoa wa Shinyanga katika kuutangaza Ushirika kuwa ni biashara.

Vyama hivyo vimeshiriki maonesho hayo kwa lengo la kuonesha fursa za kibiashara zilizoko kwenye Ushirika pamoja na uwekezaji unaofanywa na Vyama vya Ushirika katika kuwawezesha Wanaushirika na Wananchi kujikomboa kiuchumi.

Maadhimisho hayo yenye kauli mbiu "Koneksheni ndio mpango mzima" yamefanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia Novemba 04 hadi 06, 2024 mkoani Shinyanga.

Aidha, UNION zote mbili zimekuwa miongoni mwa wadhamini wakuu wa 'Shinyanga Business Forum'

## CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA KARAGWE CHAZINDUA MIRADI YA MAENDELEO



***Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) Dkt. Benson Ndiege akizindua mradi wa Maendeleo katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Karagwe (KDCU) Novemba 24, 2024 mkoani Kagera***

Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amezindua miradi ya Shilingi 899,123,987 iliyotekelezwa kwa fedha za ruzuku ya jamii zilizotokana na mauzo ya Kahawa Maalum kwa msimu wa mwaka 2022/2023 katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Karagwe (KDCU).

Dkt. Ndiege amezindua na kugawa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na Pikipiki 23 zilizogharimu Shilingi 64,400,000, Vishikwambi 40 vyenye thamani ya shilingi 37,600,000, Ununuzi wa mashuka 500 kwa ajili ya wodi ya kina mama iliyoghalimu Shilingi 11,720,650, Mtaji anzia wa SACCOS 150,000,000 na Mgao wa Vyama vya Msingi kwa ajili ya kuboresha miundo mbinu kwa kiasi cha shilingi 225,000,000.

Dkt. Ndiege amefanya uzinduzi huo tarehe 24 Novemba, 2023 Mjini Karagwe, ikiwemo kuzindua Mradi wa ujenzi wa uzio na bweni kwa Shule ya Sekondari Nyaishozi inayomilikiwa na Chama Kikuu Ushirika cha Karagwe KDCU utakaogharimu Shilingi Millioni 700 na mradi wa Kisima cha Maji katika ofisi ya KDCU ulioghalimu Shilingi Millioni 13.

Dkt. Ndiege amesema, Vyama vyote vya Ushirika

vinapaswa kufanya mambo ya kuwanufaisha wanachama wake kama ambavyo KDCU imeweza kufanya kwani chama ni mali ya wanachama na wao ndiyo wanapaswa kunufaika zaidi.

Kwa upande wake Kaimu Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika, Domitiani Robert amesema KDCU inamatarajio ya kuongeza AMCOS nyingine katika Mradi wa Kahawa Maalum ili kujenga uzalishaji endelevu na wenye tija kwa wakulima na pia ameeleza kuwa Chama kitaajiri Maafisa Ugani ili kukidhi matakwa ya mradi huo.

## MRAJIS AIPONGEZA KACU KWA KULIPA MKOPO TADB KWA AJILI YA KUNUNUA PAMBA




***Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) Dkt. Benson Ndiege (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Shinganga Novemba 23, 2023.***

Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amekipongeza Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) kwa kuweza kulipa deni la mwaka 2022 na 2023 walilokopa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa ajili ya kununua pamba mbegu.

Amesema suala la kukopa na kulipa ni jambo jema na la kupendeza ambalo linapaswa kufanywa na kila chama kinachokopa ili kujenga imani kwa wakopeshaji na Wanachama.

Mrajis ameeleza hayo tarehe 23 Novemba, 2023 alipotembelea Kiwanda cha kuchambua pamba cha KACU kilichopo mjini Kahama.

Aidha, Dkt. Ndiege amewataka viongozi wa KACU kuendelea kufanya mambo yatakayowanufaisha wanachama wao ili wanachama hao wanufaike zaidi na Ushirika wao.

# MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA....*Inaendelea*

## HAKI NA WAJIBU KWA MTEJA

***Haki kwa mteja***

| | |
|---|---|
| 1. | Kupata huduma bora bila upendeleo na kwa wakati |
| 2. | Kutoa maoni na kusikilizwa |
| 3. | Kutoa malalamiko pale ambapo hajatendewa haki na kuhusishwa |
| 4. | kusuluhisha migogoro |
| 5. | Kutunziwa nyaraka pamoja- na Kutunziwa siri |
| 6. | Kupata mrejesho wa hatua zilizochukuliwa kutokana na mlalamiko |
| 7. | Kupatiwa taarifa sahihi na kwa wakati |
| 8. | Kupokea Hati za malipo baada ya kufanya malipo |
| 9. | Kutoa ushirikiano ili kupata huduma stahiki |
| 10. | Kutoa takwimu, taarifa sahihi na kwa wakati pindi zinapohitajika |
| 11. | Kutokutoa au kupokea rushwa |

| | **WAJIBUKWA MTEJA** |
|---|---|
| 1. | Kuzingatia taratibu na miongozo yaTaasisi. |
| 2. | Kuwaheshimu watumishi waTaasisi |
| 3. | Kutoa ushirikiano ili kupata huduma stahiki |
| 4. | Kutoa takwimu, taarifa sahihi na kwa wakati pindi zinapohitajika |

***MREJESHO WA UTOAJI HUDUMA***

Maoni yako ni muhimu sana katika kuboresha huduma zetu, hivyo, tungependa kupata maoni au malalamiko yako kuhusiana na huduma zetu kwa njia zifuatazo: -

1. Barua kwa kuwasilisha ofisini au sanduku la Posta.
2. Sanduku la maoni.
3. Barua pepe, Tovuti, Simu na mitandao ya kijamii.
4. Kuonana na Uongozi au Mkuu wa Idara husika au Mrajis Msaidizi wa Mkoa husika.

Tutazingatia na kushughulikia malalamiko, maoni na ushauri haraka iwezekanavyo mara yatakapotufikia. Siku zote tunaamini mteja ni nguzo muhimu kwa maendeleo yaTaifa.

Aidha, Mkataba huu unaweza kuhuishwa endapo yatatokea mabadiliko ya Kisiasa, Kisera, Kisheria na Kiuchumi.

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania inahitajika kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwenye Menejimenti ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji kwa ajili ya kuboresha huduma na mahusiano na wateja. Taarifa hiyo itatoa majibu kwa malalamiko na maoni yaliyotolewa na wateja. Taarifa zitatolewa kwa kipindi cha robo mwaka, nusu mwaka na mwaka au pale inapohitajika

***UTAMBULISHO WA TAASISI NA NJIA ZA MAWASILIANO***

Makao Makuu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika yanapatikana Mtaa wa Kuu; Muda wa kazi kuanzia saa 1:30 Asubuhi hadi 9:30 Alasiri na Mawasiliano yote yafanyike kwa njia ya Posta, Barua Pepe, Simu na Sanduku la Maoni liliiopo katika ofisi za Tume Makao Makuu Anwani yetu ni:-

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC),

17 Barabara ya Nyerere 41101 Uhuru Dodoma,
S.L.P 201, **DODOMA**

**Simu:** + 255 026-23-22456

**Simu ya Bure:** 0800110105/0800110109

**Barua Pepe:** ushirika@ushirika.go.tz

**Tovuti:** www.ushirika.go.tz

ANUANI ZA OFISI ZA WARAJIS WASAIDIZI WA MIKOA TANZANIA BARA

| | |
|---|---|
| Mrajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa wa Dodoma S.L.P914 DODOMA BaruaPepe: mrajis.dodoma@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa waTabora S L P 315 TABORA BaruaPepe: mrajis.tabora@ushirika.go. tz |
| Mrajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa wa Kigoma SLP125 KIGOMA BaruaPepe: mrajis.kigoma@ushirika.go.tz | Msajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa wa Manyara S L P 310 BABATI BaruaPepe: mrajis.manyara@ushirika.g o.tz |
| Mrajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa waArusha S.L.P.3050 ARUSHA BaruaPepe: marajis.arusha@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa wa Mtwara S L P 235 MTWARA BaruaPepe: mrajis.mtwara@ushirika.g o.tz |
| Mrajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa wa Mara | Mrajis Msaidizi waVyama vya Ushirika, Mkoa wa Simiyu |

| | |
|---|---|
| S L P 299 MUSOMA BaruaPepe: mrajis.mara@ushirika.go.tz | S L P 136 BARIADI BaruaPepe: mrajis.simiyu@ushirika.go.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Lindi S L P 668 LINDI BaruaPepe: mrajis.lindi@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Iringa S L P 858 IRINGA BaruaPepe: mrajis.iringa@ushirika.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Katavi S L P 544 MPANDA BaruaPepe: mrajis.katavi@ushirika.tz | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Kagera S L P 299 BUKOBA Barua Pepe: mrajis.kagera@ushirika.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Rukwa S L P 128 SUMBAWANGA Barua Pepe: mrajis.rukwa@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Dar es salam S L P 5429 DAR ES SALAAM Barua Pepe: mrajis.daresSalaam@ushirika.go.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Pwani | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Ruvuma |

| | |
|---|---|
| S L P 3080 KIBAHA Barua Pepe: mrajis.pwani@ushirika.go.tz | S L P 74 SONGEA Barua Pepe: mrajis.ruvuma@ushirika.go.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro S L P 5095 MOSHI Barua Pepe: mrajis.kilimanjaro@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Singida S L P 5 SINGIDA Barua Pepe: mrajis.singida@ushirika.go.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Geita S L P 25 GEITA Barua Pepe: mrajis.geita@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Tanga S L P 3070 TANGA Barua Pepe: mrajis.tanga@ushirika.go.tz |
| Mrajis Msaidizi wa vyama vya Ushirika Mkoa wa Mbeya S L P 754 MBEYA Barua Pepe: mrajis.mbeya@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Songwe S L P 23 MBOZI Barua Pepe: mrajis.songwe@ushirika.go.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Morogoro | Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika, Mkoa wa Shinyanga |

| | |
|---|---|
| S L P 650<br><br>MOROGORO<br><br>Barua Pepe:<br><br>mrajis.morogoro@ushirika.go.tz | S L P 320<br><br>SHINYANGA<br><br>Barua Pepe:<br>mrajis.shinyanga@ushirika.go.tz |
| Mrajis Msaidizi wa Vyama vya<br><br>Ushirika, Mkoa wa Mwanza<br><br>S L P 119 MWANZA<br><br>Barua Pepe: mrajis.mwanza@ushirika.go.tz | Mrajis Msaidizi wa Vyama<br>vya Ushirika, Mkoa wa Njombe S L P 1054 NJOMBE<br><br>Barua Pepe:<br>mrajis.njombe@ushirika.go.tz |



TANZANIA CO-OPERATIVE DEVELOPMENT COMMISSION

TCDC

Together We Build Our Economy

# USHIRIKA

Pamoja Tujenga uchumi


MAKAO MAKUU YA TUME

Mtaa wa Kuu, S.L.P 201 Dodoma

+255 026 - 2322456

+255 026 - 2321973

ushirika@ushirika.go.tz

www.ushirika.go.tz

ushirika_tcdc

@ushirika_tcdc

Tume ya Maedeleo ya ushirika